ISSN 0856 – 034

*Supplement No. 38* *26th September, 2022*

## *SPECIAL SUPPLEMENT*

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.38 Vol. 103 dated 26th September, 2022*
*Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government*

TANGAZO LA SERIKALI NA 583B. la tarehe 26/9/2022

SHERIA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI
(SURA YA 268)

# HATI

*(Imetolewa chini ya vifungu vya 24(3) na 16B)*

HATI YA UANZISHWAJI WA DAFTARI LA MAWAKILI WA SERIKALI YA MWAKA 2022

Jina

**1.** Hati hii itajulikana kama Hati ya Uanzishwaji wa Daftari la Mawakili wa Serikali ya mwaka 2022.

Tafsiri

**2.** Katika Hati hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo:

"Daftari la Mawakili" maana yake ni Daftari la Mawakili wa Serikali lililoanzishwa kwa mujibu wa Hati hii;

"mwanasheria" maana yake ni mtu aliyeajiriwa katika utumishi wa umma kama mwanasheria kutekeleza majukumu ya uanasheria na inahusisha Afisa Sheria;

Sura ya 268

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

"Wakili wa Serikali" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria.

Daftari la Mawakili wa Serikali

**3.**-(1) Kutakuwa na Daftari la Mawakili wa Serikali ambalo litakuwa na majina ya watu wote walioajiriwa katika utumishi wa umma kama wanasheria kutekeleza majukumu ya uanasheria.

(2) Daftari la Mawakili litatunzwa na kupatikana katika kikoa cha https://oagmis.agctz.go.tz na litakuwa wazi kwa upekuzi na rejea ya mtu yeyote.

Mpangilio wa nambari za

**4.**-(1) Nambari za uwakili katika Daftari la Mawakili zitatolewa kwa mpangilio utakaozingatia muda wa utumishi wa

uwakili

mwanasheria.

(2) Muda wa utumishi kwa mwanasheria aliyeajiriwa kama mwanasheria utahesabiwa kuanzia tarehe ya kuajiriwa kama mwanasheria.

(3) Muda wa utumishi kwa mwanasheria aliyebadili kada utahesabiwa kuanzia tarehe ya kubadili kada kuwa mwanasheria.

Nambari maalum za uwakili

**5.-**(1) Bila kujali masharti ya aya ya 4, kutakuwa na nambari maalum za uwakili kwa wanasheria wafuatao:

(a) Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye atakuwa nambari 01;
(b) Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye atakuwa nambari 02;
(c) Mkurugenzi wa Mashtaka, ambaye atakuwa nambari 03;
(d) Wakili Mkuu wa Serikali, ambaye atakuwa nambari 04;
(e) Mwandishi Mkuu wa Sheria, ambaye atakuwa nambari 05;
(f) Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, ambaye atakuwa nambari 06; na
(g) Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, ambaye atakuwa nambari 07.

(2) Wanasheria walioainishwa katika aya ndogo ya (1) watashikilia nambari hizo kwa kipindi watakachokuwa wanahudumu katika nafasi husika.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), wanasheria waliopewa nambari maalum wataendelea kuwa na nambari zao zilizotolewa kwa kuzingatia muda wa utumishi kama wanasheria.

Hadhi na mamlaka ya Mawakili wa Serikali

**6.-**(1) Wanasheria wote walioingizwa katika Daftari la Mawakili watakuwa Mawakili wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 24(3) cha Sheria na kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (2), watakuwa na haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika mahakama zote za Jamhuri ya Muungano.

(2) Pamoja na majukumu mengine yaliyoainishwa na Sheria nyingine yoyote, Mawakili wa Serikali watakuwa pia na uwezo wa-

(a) kutoa ushauri kwenye masuala ya kisheria ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu uhakiki wa mikataba kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(b) kushiriki katika uandishi wa sheria na hati mbalimbali za kisheria kwa kuzingatia mwongozo na maelekezo ya Mwandishi Mkuu wa Sheria;
(c) kuendesha mashauri ya jinai baada ya kupewa hati

maalum ya kukasimiwa madaraka hayo na Mkurugenzi wa Mashtaka;

(d) kuendesha mashauri ya madai baada ya kupewa hati maalum ya kukasimiwa madaraka hayo na Wakili Mkuu wa Serikali;

(e) kushiriki katika majadiliano kwa niaba ya Serikali baada ya kuteuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(f) kutoa huduma za kuthibitisha nyaraka na kushuhudia viapo kwa mujibu wa Sheria husika; na

(g) kutekeleza jukumu lingine lolote kama takavyoelekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Uthibitisho wa uwakili

**7**.-(1) Uwepo wa jina la mwanasheria yeyote katika Daftari la Mawakili utakuwa uthibitisho kamili kuwa mtu huyo ni Wakili wa Serikali.

(2) Majukumu ya kisheria yaliyoainishwa katika aya ya 6 hayatatekelezwa na mtu yeyote ambaye jina lake halipo katika Daftari la Mawakili.

Kuondolewa katika Daftari

**8**.-(1) Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataondoa jina la mtu yeyote katika Daftari la Mawakili endapo mwanasheria husika-

(a) amefariki;

(b) ameacha kazi ya uanasheria katika utumishi wa umma; au

(c) amebadili au amebadilishwa kada.

(2) Kwa madhumuni ya aya ndogo ya (1), mwajiri wa mwanasheria atapaswa kumtaarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndani ya kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya kutokea kwa jambo lolote kati ya yaliyoainishwa katika aya ndogo ya (1).

Kufutwa kwa Notisi TS Na. 1011 la 2020

**9**. Notisi ya Uteuzi wa Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali inafutwa.

Dodoma
26 Septemba, 2022

ELIEZER MBUKI FELESHI
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*